# Serikali yakusanya takwimu za vifaa vya uvuvi

**Na Nashon Kennedy, Mwanza**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kwa kushirikiana na Wizara ya Uvuvi na Mifugo na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), limeanzisha sensa maalumu ya utambuzi wa vifaa vidogo vinavyotumika kwenye shughuli za uvuvi kwenye mito, maziwa makubwa na kwenye bahari ya hindi hapa nchini.

Akizungumza jana jijini hapa, Ofisa Mfawidhi wa TASAC Mkoa wa Mwanza, Hezron Lusangija alisema sensa ya vifaa hivyo vinavyotumika kwenye shughuli za uvuvi, boti na mitumbwi lililoanza rasmi Oktoba 4 mwaka huu na kumalizika Novemba 3 mwaka huu lina lengo la kupata takwimu sahihi za vifaa vya uvuvi nchini.

Alisema sensa hiyo ambayo ni ya kwanza kuanzishwa nchini, ilitanguliwa na mafunzo maalumu kwa maofisa uvuvi nchini na wadau katika tasnia ya uvuvi kama sehemu ya kuwajengea uwezo kujua umuhimu wake kwa maendeleo ya nchi.

"Sensa hii ya vifaa vya uvuvi ni muhimu sana katika ukuaji wa maendeleo katika nchi yetu, serikali inahitaji kupata takwimu sahihi za vyombo vya majini vinavyotumiwa na wavuvi ili kubaini ustawi wao na changamoto zinazowakabili, lakini pia kuwa na kanzidata kwa ajili ya shughuli za sekta ya uvuvi nchini," alisema.

Alisema tayari kwa Mkoa wa Mwanza wameshafanya sensa ya vifaa hivyo vya majini kwa mialo 54 kati ya mialo 74 kwa ushirikiano na wataalamu kutoka Ofisi ya NBS Dodoma, ofisa uvuvi mmoja kutoka kila halmashauri.

Mtakwimu kutoka NBS, Festo Mwemutsi alisema Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepiga hatua kubwa katika kutoa takwimu kwa wakati ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki kwenye maeneo ya kisera na mipango.

Alisema takwimu za sensa zinapatikana kwa haraka kutokana na kukusanywa kwenye vishikwambi kwa gharama nafuu.

Scanned with CamScanner

# Zana haramu za uvuvi zakamatwa

**Na ALODIA BABARA**, *Muleba*

ZANA haramu za uvuvi zenye thamani ya sh. milioni 16 na samaki tani sita wenye thamani ya sh. milioni 10 ambao walivuliwa kwa zana hizo, wamekamatwa wilayani hapa mkoani Kagera baada ya kufanyika doria katika Ziwa Victoria na Ziwa Burigi.

Akizungumza kuhusu tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Muleba ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya, Toba Nguvila, aliwasihi wavuvi haramu kuacha mara moja biashara hiyo.

"Uvuvi haramu unadhoofisha uvuvi endelevu, wavuvi hawa wana mtandao mkubwa. Waliokamatwa ni mabingwa wa kuingiza zana haramu kupitia mipaka mbalimbali kutoka nchi za nje kuwawezesha wavuvi haramu waliopo ndani ya nchi," alisema.

Alibainisha kuwa mtandano wa wavuvi hao haramu ni mkubwa, unahitaji umakini kuufatilia na unahitaji nguvu kubwa kuwabaini wavuvi hao," alieleza.

Alitoa rai kwa wavuvi wanaojishughulisha na uvuvi haramu, wafanye shughuli zao kihalali kwa kutumia nyavu zilizothibitishwa na serikali ambazo hazileti madhara kwa mazalia ya samaki.

Kwa upande wake, Ofisa Uvuvi Mkoa wa Kagera, Elifaz Mkama, alisema kutokana na Sheria ya Uvuvi namba 22 ya mwaka 2003, nyavu haramu na kokoro zinapokamatwa, mvuvi aliyehusika anapewa fomu ambayo wataalamu wa uvuvi wanapima zana haramu ili kuhakikisha kama hazifai kuvua samaki.

Alisema baada ya vipimo hivyo, wavuvi hao waliokamatwa watatakiwa kulipa faini au kupelekwa mahakamani.

Mkama alisema kwa upande wa samaki aina ya sangara, hairuhusiwi kuvuliwa chini ya mita 50 au 48, ambapo anapokamatwa mvuvi amevua samaki wa ukubwa huo, anapelekwa mahakamani kwa ushahidi wa ofisa uvuvi.

**UVUVI**

## KIPIMO

Hairuhusiwi kuvua sangara chini ya mita 50 au 48, atakayekamatwa kukiuka sheria hupelekwa mahakamani.

Scanned with CamScanner


Alhamisi, Oktoba 28, 2021 MWANANCHI.CO.TZ ISSN 0856-7573 NA.7752 BEI: TSH 1,000, KSH 60

# Tishio la ukame




## >>TMA yatabiri ukame kuathiri sekta nyeti nchini, zimo afya, nishati, mifugo na uvuvi

## >>Wafugaji waanza kujipanga, wasomi waitaka Serikali kuhifadhi chakula



**AFYA:** Kuzorota kwa huduma ya majisafi na salama kunaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko ambayo hubuka na athari nyingi.



**MAMLAKA ZA MAJI:** Zimeonywa kuwa kutakuwa na uhaba kwenye vyanzo hivyo vilivyopo kwa sasa vinatakiwa kulindwa dhidi ya uharibifu unaoweza kuleta madhara zaidi.

Mamlaka husika zinashauriwa kuchukua hatua stahiki za kupunguza athari hizi kwa kuwahimiza wananchi

Scanned with CamScanner